# CLASS 6 HOLIDAY HOMEWORK TERM 2 2020

# KISWAHILI

## JUMA LA KWANZA - JUMATATU.

**A. Tegua vitendawili hivi.**

1. Kutoa ni kuongeza. ______________________
2. Achora lakini hajui achoracho. ______________
3. Nikigongwagongwa wanangu hutoka. __________
4. Nnne juu ya nne ameandika nne. ______________
5. Nyumbani mwangu hamkosekani unga______________

**B. Tambua maana ya istiara hizi.**

1. Kwao ni jela . -______________________________________
2. Yeye ni kasuku. ______________________________________
3. Musa ni lumbwi. ______________________________________
4. Kwetu ni jerahanamu. __________________________________
5. Baba yangu ni simba. __________________________________

## JUMA LA KWANZA - JUMANNE.

**A. Kamilisha salamu hizi.**

1. Ndoto njema ______________________.
2. Lala unono ______________________ .
3. Alamsiki ______________________ .
4. Salaam aleikum ______________________ .
5. Sabalkheri ______________________ .

**B. Tuma kiambishi 'ndi' ifaavyo.**

1. Mimi __________ niliyetumwa.
2. Wewe __________ uliyekosa.
3. Yeye __________ aliyeitwa.
4. Sisi __________ tuliojityolea.
5. Hiki __________ kilichoibwa.

## JUMA LA KWANZA - JUMATANO

**Andika vitenzi hivi katika hali ya kutendewa na kutendua.**

| | Kitenzi | Kutendewa | Kutendua |
|---|---|---|---|
| 1. | Panga | ________ | ________ |
| 2. | Choma | ________ | ________ |
| 3. | Fumba | ________ | ________ |
| 4. | Anika | ________ | ________ |
| 5. | Waza | ________ | ________ |

**Kamiliosha katika hali ya kutendeka.**

1. Shamba lililimwa ________.
2. Chakula kilipikwa ________.
3. Nyumba ilipambwa ________.
4. Picha ilichorwa ________.
5. Nyama ilisagwa ________.

## JUMA LA KWANZA - ALHAMISI

**A. Kamilisha tanakali zifuatazo.**

1. Musa alianguka chini ________.
2. Shilingi ilianguka sakafuni ________.
3. Mkoba ulianguka matopeni ________.
4. Wairimu alipoingia wanafunzi alinyamaza ________ na kutega masikio yao ________.
5. Mzee mlafi alikila chakula ________.

**B. Tambua vikembe vya viumbe mbalimbalimbali.**

1. Nzi ________ au ________.
2. Chura ________.
3. Nyuki ________.
4. Bata ________.
5. Samaki ________.

## JUMA LA KWANZA - IJUMAA.

**Andika kifungu hiki upya ukitumia neno mkeka.**

Juzi mwalimu wangu alinileteа kifutio kipya. Kifutio chenyewe kilikuwa kizuri sana. Kilikuwa kifutio ambacho sijawahi kukiona hapo awali. Kwangu kilinivutia, nikakipenda na kuapa kukitunza vizuri. Nilimwomba aniletee kingine niwe navyo viwili. Nitafurahi kuvitumia vyote viwili. Cha kwanza kilikuwa chekundu na hivyo basi nisingetaka vyote viwe vyekundu . Je, unadhani cha pili kitakuwa na rangi gani ? Je, umewahi kuwa na chako kisicho cha wengine ?

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

## JUMA LA PILI - JUMATATU

**A. Tumia viashiria radidi.**

1. Mtoto huyu ______________________.
2. Kamata hili ______________________.
3. Shule hii ______________________.
4. Kusoma huku ______________________.
5. Maji haya ______________________.

**B. Msamiati mseto.**

1. Kipindi cha miaka kumi huitwa ______________________.
2. Kipindi cha miaka elfu moja huitwa kikwi au ______________________.
3. Maneno yenye maana sawa huitwa ______________________.
4. Maneno yenye matamshi sawa huitwa ______________________.
5. Maneno yenye maana zaidi ya moja huitwa ______________________.

## JUMA LA PILI - JUMANNE

**A. Tumia – ingine.**

1. Gari - ______________________________.
2. Mswaki - ______________________________.
3. Dawa - ______________________________.
4. Miwani - ______________________________.
5. Siku - ______________________________.

**B. Kosoa sentensi zifuatazo.**

1. Vyupa vyenyewe vimevunjika.

______________________________

2. Mimi ndiye daktari mkuu.

______________________________

3. Mtoto ambaye aliyetumwa si huyu.

______________________________

4. Wema inayozungumziwa ni hii.

______________________________

5. Mwalimu yule hapendi madawa yaliyotiwa kwenye makaratasi machafu.

______________________________

## JUMA LA PILI - JUMATANO

**Toa maana tatu za maneno yafuatayo.**

1. Kaa : (a) ______________________________
   (b) ______________________________
   (c) ______________________________

2. Panda :(a) ______________________________
   (b) ______________________________
   (c) ______________________________

3. Kata (a) ______________________________
   (b) ______________________________
   (c) ______________________________

4. Chupa : (a) ______________________

(b) ______________________

(c) ______________________

5. Chuma : (a) ______________________

(b) ______________________

(c) ______________________

## JUMA LA PILI - ALHAMISI

**Unda nomino kutokana na sifa hizi.**

| Sifa (kivumishi) | Nomino |
|---|---|
| 1. zuri | ______________ |
| 2. baya | ______________ |
| 3. ema | ______________ |
| 4. eusi | ______________ |
| 5. dhaifu | ______________ |

## JUMA LA PILI - IJUMAA

**A. Andika sentensi tano ukitumia kiambishi 'ki' cha masharti.**

1. ______________________
2. ______________________
3. ______________________
4. ______________________
5. ______________________

**B. Kanusha sentensi hizi.**

1. Huyu ni seremala.

______________________

2. Wewe u mzima.

______________________

3. Kusoma kwako kulimfaa.

______________________

4. Ukiniita nitaitika.

______________________________________________

5. Mzee huyo amekunywa dawa zinazolevya.

______________________________________________

## JUMA LA TATU - JUMATATU

**A. Kamilisha methali zifuatazo.**

1. Baada ya dhiki ________________ .
2. Mgaagaa na upwa ________________ .
3. Matikiti na ________________ .
4. Usiache mbachao ____________ .
5. Adhabu ya ________________ .

**B.**

1. Mtunzi wa mashairi anaitwa ________________________________.
2. Kifungu katika ushairi huitwa ________________________________.
3. Shairi la mishororo huitwa:
   a. Mitatu ________________________.
   b. Minne ________________________.
4. Mshororo wa mwisho unaorudiwa kila ubeti huitwa ____________ au ____________ .
5. Mstari wa mwisho katika shairi la tarbia huitwa
   ________________________________ .

## JUMA LA TATU - JUMANNE

**A. Andika sentensi hizi katika usemi wa taarifa.**

1. "Ukiniita nitaitika, " mama akasema.

______________________________________________

2. " Njooni nyote hapa, " Askari akasema.

______________________________________________

3. "Nitasafiri kesho jioni ili nikamwone," Babu akasema.

______________________________________________

4. "Jongea hapa ukitabasamu sasa hivi," Daktari akamwambia Leita.

_______________________________________________

5. "Ukija nitakutembeza huku kwangu, " Mwenyeji akamwambia mgeni.

_______________________________________________

**B. Andika akisami hizi kwa maneno.**

1. $^2/_3$ – ____________________ 2. ¾ – ____________________
3. $^7/_8$ – ____________________ 4. $^2/_9$ – ____________________
5. $^5/_6$ – ____________________

## JUMA LA TATU - JUMATANO

**A.**

1. Mshukiwa akikamatwa huwa tunasema ametiwa nguvuni au ____________________.
2. Chumba anachofungiwa mshukiwa katika kituo cha polisi huitwa ________________ .
3. ____________________ ni mtetezi wa mteja katika mahakama.
4. ________________ ni mahali ambapo mshtaki, mshtakiwa, wakili na wengineo husimama mahakamani.
5. ________________________ hutoa uamuzi mahakamani . Pia huitwa jaji.

**B. Kamilisha kwa kutumia kiulizi kilicho mabanoni ifaavyo.**

1. Watoto __________________ watatuzwa ? **(gani)**
2. Vipepeo ___________________ mliopata ? **( gani)**
3. Nilipanda miti ________________________? **(-pi)**
4. Madarasa ___________________ yaliyojengwa juzi ? **(gani)**
5. Mikunga ___________________ mliovua tangu juzi ? **(ngapi)**

## JUMA LA TATU - ALHAMISI

**A. Taja ngeli , umoja na wingi wa maneno haya.**

| | **Neno** | **Ngeli** | **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Chai | __________ | ____________ | ________________ |
| 2. | Karatasi | __________ | ____________ | ________________ |
| 3. | Chupa | __________ | ____________ | ________________ |
| 4. | Miwani | __________ | ____________ | ________________ |
| 5. | Migodi | __________ | ____________ | ________________ |

6. Mtume ________ ________ ________
7. Bata ________ ________ ________
8. Wenzo ________ ________ ________
9. Ubao ________ ________ ________
10. Jiko ________________________________

---

**JUMA LA TATU - IJUMAA**

**A.**

1. Kimelea cha kuku hasa mahali ambapo kuku ameatagia mayai ni ______________.
2. Kimelea kinachoweza kupatikana kwenye nywele ni ______________________.
3. ________________ ni kimelea kinachosababisha maradhi ya malale.
4. ________________ ni kimelea kinachofyonza damu katika mwili wa binadamu.
5. ______________ husababisha maradhi ya tauni.

**B. Toa maana tatu za neno ala.**

1. a). ________________________________________
   b). ________________________________________
   c). ________________________________________

2. Kisu kinachotiwa kwenye mtutu / mdomo wa binduki huitwa ____________________.

3. ______________________ ni kisu chenye makali pande zote mbili.
4. ____________________ ni zana ya kivita inayopita chini ya maji.
5. Chagua neno lisilofaa katika kundi hili.

   **Sime, parapanda, singe, kombora.**

E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

# JARIBIO LA KWANZA

***Soma vifungu vifuatavyo, vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila pengo umepewa majibu manne. Chagua jawabu lifaalo zaidi.***

Mvua ilikuwa ___1___ usiku kucha. Maji ___2___ yakawa yamezagaa kila ___3___ .Jambo la kusikitisha ni kuwa baadaye ___4___ walianza kuzaana kwa wingi na kusababisha watu ___5___ malaria. ___6___ nyingi za hospitali zilijaa wagonjwa waliolazwa kutokana na ugonjwa ___7___. Mwalimu alituambia kuwa mvua ni muhimu lakini ikinyesha zaidi huleta ___8___ . Hata hivyo, ikikosa kunyesha husababisha ___9___.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. limenyesha | B. imenyesha | C. umenyesha | D. kumenyesha |
| 2. | A. mwingi | B. nyingi | C. mingi | D. mengi |
| 3. | A. mahari | B. hali | C. mahali | D. mali |
| 4. | A. mbu | B. mbung'o | C. viroboto | D. mchwa |
| 5. | A. kugonjeka | B. kuungua | C. kupona | D. kuugua |
| 6. | A. Wadi | B. Wodi | C. Vitanda | D. Nyumba |
| 7. | A. huwo | B. hayo | C. huo | D. hao |
| 8. | A. maafa | B. manufaa | C. faida | D. makosa |
| 9. | A. mafuriko | B. kipupwe | C. baridi | D. ukame |

Mtoto ___10___ yule ana haki ___11___ kupewa elimu. Serikali yetu inatoa elimu ya bure ___12___ shule ___13___ umma. Mzazi ambaye ataripotiwa kwa kukosa kumpeleka mwanawe shuleni ___14___ na kula kalenda ___15___.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 10. | A wowote | B. yoyote | C. yeyote | D. mwingine |
| 11. | A. ya | B. wa | C. la | D. za |
| 12. | A. kwa | B. katika | C. ndani mwa | D. katai ya |
| 13. | A. yote ya | B. yote za | C. zote ya | D. zote za |
| 14. | A. atatiwa mbaroni | B. atachana mbuga | C. atafua dafu | D. atakata kamba |
| 15. | A. kizimbani | B. barazani | C. gerezani | D. zahanatini |

***Kuanzia nambari 16 mpaka 30, jibu kila swali kulingana na maagizo.***

16. Mtu anapotaka kuvuna mchele hustawisha
    A. mpunga B. mgomba
    C. mibibo D. mibuni.

17. Andika wingi wa sentensi ifuatayo
    **Barabara hiyo itatiwa lami.**
    A. Mabarabara hayo yatatiwa lami.
    B. Barabara hizo zitatiwa lami.
    C. Mabarabara hizo zitatiwa lami.
    D. Barabara hayo yatatiwa lami

18. Chagua methali inayowaonya wazazi wasiogope kuwaelekeza watoto wao?
    A. Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu.
    B. Uchungu wa mwana aujuaye ni mzazi.
    C. Mchelea mwana kulia hulia mwenyewe.
    D. Mtaka cha mvunguni sharti ainame.

19. Nomino pua, shingo na ndizi hupatikana katika ngeli ipi?

A. KI-VI B. LI-YA

C. I-ZI D. U-YA

20. Maskani yapi yamekosewa?

A. Mchwa - kichuguu.

B. Kuku-kizimba.

C. Ng'ombe-zeriba.

D. Kiwavi - kiota.

21. Orodha ipi inayoonyesha viashiria pekee?

A. Angu, etu, enu, ake.

B. Huyu,vile,hivyo,haya.

C. Gani,tamu,bora,mpya.

D. enye,enyewe,ote,o-ote.

22. Mtu akikuaga '**Ndoto njema**" nawe utamjibu

A. ya mafanikio

B. buriani

C. jaala

D. Inshallah

23. Tunasema, Anguka pu! lakini nyooka

A. Nyoo! B. Nywee!

C. Ka! D. Twaa!

24. Vazi linalovaliwa na makanika ili mavazi yao yasichafuke huitwa

A. kanchiri B. surupwenye

C. kizibao D. kabuti

25. Tumia kisisitizi **-ndi-** kwa usahihi.

A. Maji haya ndio yaliyomwagika.

B. Maji haya ndilo yaliyomwagika.

C. Maji haya ndiyo yaliomwagika.

D. Maji haya ndiyo yaliyomwagika.

26. Mstari mmoja wa maneno katika shairi huitwa

A. Kibwagizo B. mizani

C. mshororo D. sentensi.

27. Sentensi ipi ina kivumishi cha idadi?

A. Tunda la pili limeiva.

B. Shule zote zimefunguliwa.

C. Saa yangu imepoteza majira.

D. Mji huo una wakazi wazuri.

28. Tunasema mrefu kama mlingoti na mwaminifu kama

A. malaika B. jua

C. mchana D. usiku.

**29.** Malipo ya kuachiliwa kwa muda huku kesi ikiendela ni

A. arshi B. riba
C. faini D. dhamana

**30.** Akisami $^3/_8$ kwa maneno huitwa

A. thuluthi tatu B. thumni tatu
C. humusi tatu D. humusi nane

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 – 40***

Nchini Kenya dhana ya mtoto inatofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine. Katika jamii nyingi, kuna mila na desturi ambazo huashiria kuvuka kutoka utotoni kuingia utu uzima. Tutaziita mila hizi za upisho kwa sababu humpitisha mtu kutoka kiwango kimoja hadi kingine. Mtu huwa mzima pindi tu anapopitia mila na desturi za upisho. Mila na dsturi hizo za upisho huwa muhimu kwa kuwa mtu akitambuliwa kama mtu mzima hupata uhuru wa kutekeleza mambo fulani kama vile uhuru wa kuoa au kuolewa. Umri wakupitia mila na desturi za upisho hutofautiana kutegemea jamii. Mtu aliye na umri wa miaka kumi na mitatu anaweza kuwa mtoto katika jamii fulani na katika jamii nyingine akawa mzima.

Serikali ya Kenya imepitisha sheria ya kusawazisha dhana ya mtoto. Usawazishaji huo umeafikiwa kwa kutumia umri kwa mujibu wa sheria ya watoto ya mwaka wa elfu mbili na moja, mtoto ni mtu aliye na umri wa chini ya miaka kumi na minane. Hii ni kuambatana na makubaliano kuhusu haki za watoto ya mwaka wa elfu moja mia tisa tisini.

Kwa kuzingatia kigezo cha umri, mtu anapotimia umri wa miaka kumi na minane huwa amepiga hatua muhimu katika ukuaji wa mwanadamu na hivyo huwa mtu mzima. Ingawa haya ni kweli katika ujumla wake, mazingira anamokulia mtoto kama vile ya kitamaduni, kijamii na kisiasa huchangia pakubwa katika kuamua ni wakati gani mtu anapokuwa mzima.

**31.** Dhana ya mtoto hapa nchini Kenya

A. Imesawazishwa na jamii
B. huwa tofauti kwa kutegemea jamii
C. si muhimu katika jamii
D. haijulikani katika jamii.

**32.** Mtu huwa mtu mzima katika jamii fulani baada ya

A. kupitia mila na desturi za upisho
B. kuogezeka umri na kuwa mkubwa
C. kuonyesha ujasiri na bidii maishani
D. kusoma na kuhitimu mafunzo yote shuleni.

**33.** Ipi si mojawapo ya mila na desturi za upisho?

A. Tohara ya wavulana.
B. Kuwinda wanyama katika jamii fulani.
C. Kuolewa ukiwa mtoto.
D. Kung'olewa meno katika baadhi ya jamii.

**34.** Mila hizi za upisho huwa muhimu kwa kuwa

A. mtu huacha kuwaheshimu wakubwa
B. mtu hupata uhuru wa kuvunja sheria
C. mtu huanza kuogopwa na watu wote
D. uhuru wa kutekeleza mambo fulani hupatikana.

35. Si kweli kusema kwamba
A. mtu wa miaka kumi na mitatu ni mzima katika jamii zote.
B. Mtu wa miaka kumi na minane ni mzima katika baadhi ya jamii.
C. Mtu wa miaka kumi na mitatu ni mzima katika baadhi ya jamii.
D. Mtu wa mika kumi na mitatu ni mtoto katika baadhi ya jamii.

36. Sheria iliyopitishwa nchini Kenya ni ya
A. kuwafanya watoto kuwa watu wazima
B. kusawazisha dhana ya mtoto
C. kuwaonea na kuwatesa watoto
D. kuwafanyia watoto mila na desturi.

37. Kulingana na serikali mtoto huwa
A. na miaka kumi na minane
B. miaka zaidi ya kumi na minane
C. miaka chini au zaidi ya kumi na minane
D. miaka isiyofika kumi na minane

38. Sheria ya watoto ni ya mwaka wa
A. 201 B. 1996
C. 2001 D. 1990

39. Mtoto wa miaka kumi na minane huwa mtu mzima kwa sababu
A. amepitia mila na desturi za upisho
B. amepiga hatua muhimu katika ukuaji wake
C. amepata kitambulisho cha taifa
D. anaweza kuoa au kuolewa

40. Mazingira anamokulia mtu yametajwa kuwa yote haya isipokuwa
A. kimavazi B. kitamaduni
C. kijamii D. kisiasa.

***<u>Yasome makala haya kwa makini kisha ujibu maswali</u>*** **<u>41 – 50</u>**

Asubuhi moja fisi aliamka mnyonge. Alipotazama jikoni hakuona moshi ukifuka. Akajua kuwa pasipo moshi bila shaka hapana moto; na pasipo na moto **<u>staftahi</u>** haipatikani . Akajiona kama anayechezewa na ulimwengu. Akakumbuka katika enzi za ujana wake ambapo alikuwa msasi mashuhuri aliyeogopwa na paa wote. Akapiga moyo konde na kusema kuwa lazima aende kujitafutia chakula. Baada ya kunawa uso , Fisi **<u>alishika njia</u>** kuelekea msituni bila hata kuwajuza wake na wanawe asije akaamsha tumaini lao na kuwafanya watarajie chochote. Haikuchukua muda kabla ya kuziona nyayo za mnyama fulani. Akazifuata hatua chache, huku macho yake yameng'aa kwa matumaini. Akawa anaongeza mambo huku na kule. Muda si muda akasikia mroromo wa ndama mdogo.

Roho ya fisi ikachanua; akapiga kifua na kusema "Leo Mungu amemshushia mja wake neema asiyoilalia wala kuiamkia." Akafululiza hadi alipoisikia sauti hiyo iliyompa bashasha. Hakuamini macho yake alipokuta kuwa kweli ndama huyo alikuwa amefungwa kumngojea yeye. Alimtazama ndama kwa shauku kubwa akiwaza aanzie wapi. Mara wazo zuri ilimjia. "Nimetafunwa na njaa kwa karne nyingi. Naye huyu ndama amenawiri si haba, kisha kafungwa kwa kamba ambayo pia huweza kuwa mlo hata kwa simba aliyekosa nyama nitaanza kuufaidi uhodo wa kamba hii, kisha nimshughulikie ndama wangu polepole. Nitakula shibe yangu kwa siku mbili-tatu huku walio nyumbani wakidhani kua nimekuja kuwatafutia"

Ghafla fisi akajipandisha ghadhabu. Akaivamia kamba na kuanza kuitia jino huku akibwata maneno yasiyosikika ndama ambaye wakati wote huu alikuwa akisisimkwa na malaika kwa woga, alipata wokovu mwembamba kama sindano baada ya kamba kukatika. Akatundika guu begani na kumwacha fisi akilia kwa kekevu.

Wakati huu wote mzee kobe ambaye alikuwa jirani wa fisi alikuwa akimtazama kwa mbali kutoka mafichoni. Mara akajitokeza na kumwuliza fisi kilichokuwa kikimliza. Fisi, baada ya kuona fedheha alisimulia kisa chake. Kobe badala ya kumwonea fisi imani, alimwonya dhidi ya vitendo vyake vya kijinga vilivyosababishwa na tamaa . Tangu siku hiyo fisi hakuheshimiwa tena na wanyama.

**41.** Maana ya fisi kuamka akiwa mnyonge ni kuwa alikuwa

A. hana raha B. hana nguvu
C. hana uchovu D. hana hamu ya kula

**42.** **Staftahi** kulingana na kifungu ni

A. chakula cha adhuhuri
B. chakula cha jioni
C. chakula cha mchana
D. chakula cha asubuhi.

**43.** Zamani fisi anakumbuka alikuwa

A. msasi aliyejulikana B. akiwaogopa paa
C. mjaja kama sungura D. mlafi kupindukia.

**44.** Fisi **alishika njia** ndiko kusema

A. aligusa njia kwa mkono
B. alipotea njia
C. alifuata njia
D. alianza kukimbia.

**45.** Baada ya kutembea kwa muda fisi aliona

A. ndama aliyefungwa
B. kobe aliyejificha
C. paa aliyemwogopa
D. nyayo za mnyama fulani.

**46.** Inaonekana kuwa ndama yule alikuwa

A. amenenepa B. amekonda
C. amekufa D. amenona

**47.** Baada ya kuwaza na kuwazua, fisi alikata shauri gani?

A. Kumvamia ndama mara moja
B. Kuanza kula kamba
C. Kumfungua ndama kamba
D. Kumshtua ndama yule.

**48.** Fisi alitaka kumla ndama kwa siku tatu bila kurudi nyumbani kwa sababu alikuwa

A. mwoga na mjinga B. jasiri na mwerevu
C. mlafi na mchoyo D. mjinga na mwerevu

49. Fisi alipoongea na kobe alikuwa
A. ameaibika
B. amefurahi
C. amechangamka
D. ameshiba

50. Kichwa mwafaka kwa makala haya ni:
A. Polepole ya kobe humfikisha mbali.
B. Mwenye pupa hadiriki kula tamu.
C. Ujanja wa nyani huishia jangwani.
D. Jogoo la shamba haliwiki mjini.

---

# JARIBIO LA PILI

---

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi* 1 *mpaka* 15. *Kwa kila pengo umepewa majibu manne. Chagua jawabu lifaalo zaidi.***

Urafiki wa ____1____ una maana ya ____2____rafiki ____3____. Huyu ataweza kukusaidia wakati ____4____kwani wahenga walisema kuwa____5____ kwa ____6____ndiye rafiki. Lakini, jambo____7____kushangaza ni kwamba sisi ____8____ marafiki ____9____ pale wanapofikwa na shida.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. chati | B. dhati | C. hati | D. dati |
| 2. | A. kuwa | B. kua | C. kukua | D. kukuwa |
| 3. | A. mwongo | B. duni | C. mtundu | D. mwaminifu |
| 4. | A yoyote | B. yote | C. wowote | D. popote |
| 5. | A. akufaaye | B. akuitaye | C. akuokoaye | D. akuinuaye |
| 6. | A. shida | B. dhiki | C. taabu | D. kweli |
| 7. | A. za | B. wa | C. la | D. ya |
| 8. | A. huwakimbilia | B. huwakimbiza | C. huwakimbizia | D. huwakimbia |
| 9. | A. yetu | B. wetu | C. mwetu | D. zetu |

Tuliandamana na wavyele wangu ____10____mjini kuninunulia ____11____mpya ya shule. Nilikuwa na furaha ____12____. Nilijua kuwa ningejionea magari mengi na majengo ____13____ . Tuliabiri ____14____na kulipa ____15____yetu ndipo safari ikaanza.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 10. | A tangu | B. hadi | C. bali | D. katika |
| 11. | A. sare | B. suti | C. shati | D. kanchiri |
| 12 | A. mingimingi | B. bingiribingiri | C. mpwitompwito | D. rovurovu |
| 13. | A. mirefu | B. mrefu | C. ndefu | D. marefu |
| 14. | A. lori | B. manowari | C. matwana | D. ambulensi |
| 15. | A. kingilio | B. nauli | C. karo | D. masrufu |

***Kuanzia nambari* 16 *mpaka* 30, *jibu kila swali kulingana na maagizo.***

16. Chagua sentensi iliyo katika hali timilifu
A. Uji ulipoa ukanywewa
B. Uji umepoa ukanywewa
C. Uji ukipoa utanywewa
D. Uji unapopoa hunywewa

**17.** Andika wingi wa :

*Blanketi langu limelowa maji.*

A. Mablanketi yetu yamelowa maji.
B. Blanketi zetu zimelowa maji
C. Mablanketi zetu zimelowa maji
D. Blanketi zangu zimelowa maji

**18.** Akisami $\frac{5}{8}$ huitwaje?

A. Humusi nane
B. Thumni nane
C. Thumni tano
D. Humusi tano

**19.** Ugonjwa upi huathiri ngozi ya binadamu?

A. Kipindupindu  B. Choa
C. Kifuakikuu  D. Malale

**20.** Chagua sentensi yenye kivumishi cha pekee.

A. Tunda bivu limeliwa
B. Mtoto mmoja analia
C. Maji yale yamechemka
D. Ng'ombe wote wamekamwa


**21.** Alama ipi hutumika mwishoni mwa sentensi?

A. Kikomo  B. Ritifaa
C. Koma  D. Kistari kifupi

**22.** Sentensi gani imetumia '*ji*' tamati kuonyesha anayetenda jambo?

A. Ulimaji wa shamba ni mgumu
B. Mkataji wa kuni amefika
C. Mkulima amejikata mkono
D. Jitu limenikimbiza sana

**23.** Umbo lifuatalo ni



A. duara  B. mchemraba
C. mcheduara  D. pia

**24.** Tunasema msiri kama usiku na mwepesi kama

A. sindano  B. jiwe
C. mtoto  D. paa

**25.** Ndege yupi ni mdogo kuliko wengine?

A. Mbuni  B. Kipanga
C. Sigi  D. Kanga

**26.** **Kanusha:**
*Mwalimu wetu alifika mapema.*
A. Mwalimu wetu hajafika mapema
B. Mwalimu wetu hakufika mapema
C. Mwalimu wetu hatafika mapema
D. Mwalimu wetu hafiki mapema

**27.** Kamilisha kwa tashbihi ifaayo
Barabara hii imenyooka _______; haina kuruba yoyote.
A. twaa B. nywee
C. nyoo D. fwaa

**28.** Tegua kitendawili kifuatacho.
Ni changu lakini hutumiwa na wengine zaidi yangu.
A. kiti B. mkono
C. kitabu D. jina

**29.** Tumia kirejeshi '**amba**' kwa usahihi;
A. Mzazi ambaye aliyekuja ni wangu.
B. Mzazi ambaye alikuja ni wangu.
C. Mzazi aliyekuja ni wangu.
D. Mzazi ambao alikuja ni wangu

**30.** Mmea ukipata mbolea nzuri na maji
A. hukauka B. hunawiri
C. hunyauka D. hudhoofika

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali* 31 – 40**

Maisha ya kule yalishinda ya utumwa au kifungo. Mtumwa na mfungwa huwa na nafasi ya kuona nje na kutangamana na watu, japo kwa masharti. Huu ndio wakati nilipogundua kuwa **kuketi tutwe** ni vigumu kuliko kufanya kazi ngumu. Tena chumba kile kilicho jaa mwangaza kilinizuia kujua usiku na mchana, hivyo kushindwa kuyatambua majira. Upweke na mawazo mengi viliandamana. Wakati wa haja nililetewa ndoo, sawia na wakati wa kuoga. Sikuruhusiwa kuwa nje. Kitanda hakikuwa na thamani kwangu. Nilikiona kama pingu. Sikujua wakati wa kulala. Nadhani ningekaa hata muda wa siku tano bila kupata lepe la usingizi.

**Mungu si athmani**. Nilimwomba kila wakati aninusuru. Siku ya kuokolewa kwetu ilikawia mno ila hayawi hayawi huwa. Ilifika. Nilisikia kwa mbali mlio kama wa bunduki, nikajua sala yangu imetimia. Mfyatuko ule ulipofika mlangoni pa chumba changu, nilisikia sauti ya mtu aliyepigwa risasi akipiga mayowe. Nikaomba yangu ya mwisho. Kilichofuata ni kualika kwa msumeno uliokuwa ukikata kufuli la mlango wangu. Walioingia badala ya kuniangamiza walinikimbilia huku wakinikinga kama afanyavyo kuku akiwakinga vifaranga wake. Wakati huo nilikuwa nimejikunyata mvunguni mwa kitanda. Walinitolea maneno ya kunifariji. Walikuwa wamevalia sare za askari zilizofanana na za wale wa nchi yetu, thibitisho kuwa tulikuwa tumetekwa nyara na wahuni wa nchi jirani. Ilikuwa ni siku ya siku; ya kukutana na wenzangu tuliotekwa nyara pamoja miezi mitatu iliyokuwa imepita.

**31.** Maisha ya msimulizi yalishinda ya utumwani au kifungo kwa sababu
A. yalijaa taabu zaidi
B. hakulipwa chochote
C. alipigwa zaidi
D. hakuna aliyekuja kwake

32. Maana ya **'kuketi tutwe'** ni
A. kuogopa sana
B. kukaa bila kufanya lolote
C. kukaa peke yako
D. kukaa chini tu

33. Ilikuwa vigumu kujua usiku na mchana kwa kuwa
A. hakuwa na saa yoyote
B. chumbani mlijaa giza
C. alilala wakati wote
D. chumba kilijaa mwangaza

34. Kazi ya ndoo ilikuwa
A. kuchota maji na kuoga
B. kujisaidia na kuogea
C. kuogea na kufulia nguo
D. kuendea haja kubwa na ndogo tu

35. Mtu huhisi upweke wakati
A. anapoogopa
B. anapolala
C. akiwa peke yake
D. akiwa amechoka

36. Tunasema lepe la usingizi lakini _____ la maji.
A. biwi
B. tita
C. shungi
D. funda

37. Mungu si athmani kwa sababu
A. alimwokoa msimulizi
B. msimulizi alitekwa nyara
C. msimulizi aliuawa
D. msimulizi alitoroka

38. Aliyefyatuliwa risasi alikuwa nani?
A. Rafikiye mnenaji
B. Askari mmoja
C. Aliyelinda mlangoni
D. Mbwa wa askari

39. Askari walimlinda msimulizi kwa sababu
A. alikuwa kiongozi wao
B. maadui wasimdhuru
C. alikuwa mnyonge sana
D. hakujua alikokuwa

40. Msimulizi na wenzake walizuiliwa kwa muda wa takriban
- A. siku thelathini
- B. miongo mitatu
- C. wiki tatu
- D. siku tisini

***Yasome makala haya kwa makini kisha ujibu maswali 41 – 50***

Ni bayana kuwa watoto ni viumbe walio na thamani kubwa. Insani hawa wana vipawa mbalimbali na manufaa yanayoweza kunufaisha kizazi kijacho, lakini ajabu ni kwamba wavyele wengi hawapatii watoto nafasi ya kukuza vipawa na uwezo wao. Badala yake, huwapa jukumu la kujitafutia riziki maishani.

Watoto hasa wa kike wanapoajiriwa hukumbana na shida teletele. Chukua kwa mfano mtoto aliyeajiriwa kwenye familia ya takriban **adinasi** watano. Mtoto huyu anapaswa kufanya kazi hii sawa na mtu mzima.

Pili, awapo msichana huyatatiza maisha yake kwani siku hizi binadamu wamekuwa wanyama. Msichana kama huyu anaweza kupigwa anapofanya makosa ama kunyimwa chakula au mahali pa kulala, na mbali na hayo kunajisiwa. Hivyo basi, ajira ya watoto imekuwa mojawapo ya vyanzo vya ukimwi au maradhi ya zinaa.

Kwa kawaida, kijakazi anaposhawishiwa kufanya mapenzi na mwajiri wake huogopa kupigwa kalamu. Umoja wa mataifa umekuwa katika mstari wa mbele katika kupigana na ajira za watoto na umehimiza mataifa yashiriki katika juhudi za kuimarisha haki za watoto.

Licha ya juhudi hizo na mafanikio, wapo watoto ambao wameajiriwa kwa sababu ya dhiki na matatizo mengi yanayoikabili jamii. Hivyo, ni jukumu la serikali katika mataifa hayo kuona kwamba zimepitisha miswada ambayo inazuia ajira za watoto.

41. Kulingana na aya ya kwanza
- A. watoto ni viumbe muhimu
- B. watoto ni viumbe wa ajabu
- C. watoto hawana hatia yoyote
- D. watoto hawana haki zozote

42. Ni vyema kuwapa watoto nafasi ya kukuza vipawa vyao kwa sababu
- A. wana vipawa vingi kuliko wazazi
- B. wengine wao hawana vipawa
- C. wanatarajiwa kufaidi kizazi cha kesho
- D. wote wamenyimwa nafasi ya kujiendeleza

43. Wazazi wengine wamewaacha watoto
- A. kujifanyia lolote watakalo
- B. kujitafutia riziki wenyewe
- C. kujibizana na watu wazima
- D. kujua pesa mapema

44. Neno **'adinasi'** lina maana ya
- A. wanja
- B. watoto
- C. waajiri
- D. waja

**45.** Wasichana hutatizika zaidi kwa sababu

A. hawawezi kujifanyia kazi yoyote
B. wanadhulumiwa zaidi ya wavulana
C. wanapendwa kuliko wavulana
D. ni wajinga kuliko wavulana

**46.** Ipi si adhabu wanayopewa wasichana wanapokosa?

A. Kupigwa
B. Kunyimwa chakula
C. Kupewa malazi
D. Kulala nje

**47.** Kukosa kumtendea mtu haki ni

A. kumdhulumu
B. kumpendelea
C. kumwaibisha
D. kumpiga

**48.** Vijakazi hushiriki mapenzi na waajiri maadamu

A. wanapenda pesa sana
B. wanataka waolewe
C. hawana pa kuenda
D. wanahofia kuachishwa kazi

**49.** Umoja wa mataifa unatetea sana

A. ajira ya watoto
B. haki za watoto
C. vijakazi wasiajiriwe
D. vijakazi wasinyanyaswe

**50.** Watoto wengi huajiriwa kutokana na

A. shida za maisha
B. kushindwa na masomo
C. mateso ya wazazi
D. tamaa ya pesa